

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI



MANAWASA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASASI-NACHINGWEA (MANAWASA)

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA KUJITOLEA.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi Nachingwea (MANAWASA) ni Taasisi ya umma chini ya Wizara ya Maji iliyoanzishwa kupitia Tangazo la Serikali lenye **GN.No 105** ya tarehe 10 Mei 2013 ikitoa huduama kwenye Mji wa Masasi na Nachingwea, Aidha kupitia zoezi la uunganishaji wa Mamlaka (*clustering*) la mwaka 2019 Mamlaka ya Mji Mangaka iliunganishwa na MANAWASA sawa na **GN. 826** ya mwaka 2019.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi- Nachingwea (MANAWASA) anapenda kuwatangazia Watanzania wenye sifa nafasi za kazi ya kujitoa na wanatakiwa kutuma maombi kwa mchanganuo ufuatao:-

1. MCHUMI II (Nafasi 1)

1.1 SIFA ZA MUOMBAJI

Mwombaji awe na ufaulu wa elimu ya kidato nne, sita pamoja na shahada kwenye nyanja zifuatazo Uchumi, Takwimu, Idadi ya Watu na Mipango au taaluma nyingine inayoendana na iwe kutoka kwenye chuo kinachotambulika.

1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kusaidia kufuatilia na kupima ufanisi wa taasisi
- ii. Kusaidia uratibu wa uandaaji wa mikakati, malengo na bajeti na kusimamia utekelezaji wake
- iii. Kusaidia kuratibu ufuatiliaji na tathimini kwa shughuli za mamlaka
- iv. Kusaidia maandalizi ya makisio ya mapato na matumizi ya taasisi
- v. Kusaidia kufanya utabiri (forecast) juu ya mipango ya Taasisi ya muda mrefu na muda Mfupi
- vi. Kushauri maboresho ya matumizi sahihi ya rasilimali pamoja na kusaidia kubuni miradi na vyanzo mbadala vya mapato (altenative financing).
- vii. Kufanya majukumu mengine yoyote yanayohusiana na wigo wa kazi kama itakavyopangwa na Msimamizi.

1.3 MSHAHARA

Mshahara/ Posho itaipwa kwa kuzingalia Muongozo wa Malipo wa MANAWASA.

SIFA ZA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

1. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 na wasizidi miaka 35 na awe hajawahi kuajiriwa na taasisi yoyote ya umma.
2. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (*detailed Curriculum Vitae*) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu wa kuaminika.
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya elimu na taaluma vilivyothibitishwa/ hakikiwa na wakili wa Serikali, ambapo ni vyeti vya elimu ya kidato cha nne, sita na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya taaluma kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
4. Mwombaji aambatanishe kitambulisho cha Taifa au Namba ya NIDA pamoja na paspoti mbili za rangi.
5. Kazi ya kujitolea ni ya mwaka mmoja.
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU).
7. Uwasilishaji wa taarifa za kughushi wahuika watachukuliwa hatua za kisheria.
8. Kuwa tayari kufanya kazi katika kanda au eneo lolote la Mamlaka (Masasi, Nachingwea na Nanyumbu)
9. Maombi yatapokelewa kwa njia zifuatazo; Ofisi ya Masijala MANAWASA, Barua pepe na kwa njia ya sanduku la posta.
10. Mwisho wa kupokea maombi ni siku Jumatano tarehe **10.11.2026** saa **tisa na nusu** mchana
11. Barua ya maombi inapaswa kuwa imesainiwa na muombaji na kuelekezwa kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI,

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MASASI-NACHINGWEA,


(MANAWASA),

S.L.P 133,

MASASI.

Barua pepe; info@manawasa.go.tz

Imetolewa na ;



KIULA MAKALLA KINGU
MKURUGENZI MTENDAJI-MANAWASA

